**MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA TAREHE 19/11/2021**

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Ndg. Butamo Ndalahwa | - | Mkurugenzi Mtendaji(W) - Mwenyekiti |
| 2 | Ndg. Ruth N. Mwelo | - | Afisa Utumishi na Utawala (H/W) - Katibu |
| 3 | Ndg. Fatuma Kisalazo | - | Afisa Elimu Sekondari (H/W) |
| 4 | Ndg. Zahoro Thabit | - | Kny: Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (H/W) |
| 5 | Ndg. Evans Mwalukasa | - | Kaimu Mweka Hazina (H/W) |
| 6 | Ngd. Brown H. Nziku | - | Afisa Ardhi na Maliasili (H/W) |
| 7 | Ndg.Omari Mshamu | - | Afisa Manunuzi na Ugavi (H/W) |
| 8 | Ndg. Frank Mkude | - | Kaimu: Mkuu wa Idara ya Ujenzi (H/W) |
| 9 | Ndg. Sijaona Muhunzi | - | Mratibu wa Mfuko wa Kijiji(H/W) |
| 10 | Ndg.Peter Mundo | | Kny:Mwanasheria (H/W) |
| 12 | Ndg. Abel Musa | - | Kny: Mkaguzi wa ndani (H/W) |
| 13 | Dr. Ibrahim Isack | - | Mganga Mkuu (H/W) |
| 14 | Ndg. Happy Chinduli | - | Afisa Biashara (H/W) |
| 15 | Ndg.Christina Samwel | | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki (H/W) |
| 16 | Ndg. Victoria Mtengie | - | Mratibu wa UKIMWI |
| 17 | Ndg. Joseph Biruma | - | Kny: Afisa Elimu Msingi (H/W) |
| 18 | Ndg.Mwanila Sembinga | - | Kaimu A/Mtendaji M/M/Mlandizi |
| 19 | Ndg. Nicodemus Mombia | - | Afisa Wanyamapori |
| 20 | Ndg.Ombeni Msangi | - | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 21 | Ndg. Joackim Assey | - | Afisa Mipango (H/W) |
| 22 | Ndg. Mahamodu Mrutu | - | Kny: Afisa TEHAMA |
| 23 | Ndg. Maximilian E.Mtobu | - | Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (H/W) |

-

**SEKRETARIETI**

1 Ndg Adam Masinde

2 Ndg. Mariam Lambileki

**KDC.CMT.NA.05/11/01/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na aliwataka kuwa wasikivu na wepesi wa kuchangia mada, hatimaye alifungua kikao saa 04:02 asubuhi.

**KDC.CMT.NA.05/11/02/2021: KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 19/11/2021**

Wajumbe walizipitia agenda sita (06) zilizowasilishwa na Katibu. Wajumbe kwa kauli moja waliridhia ziwe agenda halali za kikao hicho.

**KDC.CMT.NA.05/11/03/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA MENEJIMENTI 12/10/2021**

Wajumbe waliupitia muhtasari ukurasa kwa ukurasa bila kufanya marekebisho yoyote, wajumbe waliridhia muhtasari huo uthibitishwe na usainiwe ili uwe kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**KDC.CMT.NA.01/11/04/2021: MAPOKEZI YA FEDHA TSH.90,000,000.00 ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO -19 KWA AJILI YA UJENZI WA KITUO CHA AFYA**

Scanned with CamScanner

Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa kuwa, tarehe 19/11/2021 Halmashauri imepokea fedha Tshs. Shilingi **90,000,000.00**, kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba 1 itakayoweza kutumiwa na watumishi 3 wa Idara ya Afya.

Taarifa ilipokelewa na wajumbe walijadili yafuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa fedha hizo zimeletwa lengo likiwa ni kuboresha makazi ya watumishi, wao kama Menejimenti wajipange kuhakikisha zinasimamiwa vizuri. Aidha Idara ya Ujenzi, Kitengo cha Ununuzi na Ugavi na Idara ya Afya kwa kushirikiana na Afisa Mipango (W) wahakikishe ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha miradi yote inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa na ikamilike kwa wakati.

Wajumbe kwa pamoja baada ya majadiliano hayo waliridhia utekelezaji uanze kwa wakati.

**KDC.CMT.NA.01/11/05/2021: MWONGOZO NA MATUMIZI YA "FORCE ACCOUNT"KATIKA MAMLAKA ZA CHINI (LOWER LEVEL AUTHORITY)**

Kaimu Afisa Ununuzi na Ugavi aliwasilisha taarifa taarifa ya mwongozo na matumizi ya "force account" katika mamlaka za chini.

Wajumbe walipokea taarifa na walishauri ipelekwe kwenye kikao cha kamati ya fedha na mipango.

**KDC.CMT.NA.01/11/06/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwashukuru wajumbe kwa ushauri walioutoa na aliagiza kila mtu atimize wajibu wake na washirikiane katika utekelezaji wa miradi ya UVIKO- 19 ili iweze kukamilika kwa wakati na alifunga kikao saa 06:10 Mchana.

***MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA:***

BUTANO N. NDALAHWA
**JINA LA MWENYEKITI**

**SAHIHI:** [signature]

**TAREHE:** 10/12/2021

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KIBAHA

RUTH N. MWELO
**JINA LA KATIBU**

**SAHIHI:** [signature]

**TAREHE:** 10-12-2021



Scanned with CamScanner